

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU TANGAZO LA  
MSAMAHA NA USALIMISHAJI WA SILAHA KWA WAMILIKI WA  
SILAHA KINYUME NA SHERIA**

**Ndugu wanahabari,**

1. Nchi nyingi wanachama wa Umoja wa Mataifa, ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zimesaini na kuridhia mikataba, Itifaki, maazimio na makubaliano mbalimbali ya Kuzuia Uzagaaji wa Silaha Ndogo na Nyepesi. Moja ya makubaliano hayo ni Makubaliano ya Umoja wa Mataifa yaliyofanyika mwezi Julai 2018 kuhusu udhibiti wa uzagaaji wa silaha haramu. Uzagaaji wa silaha haramu duniani umekuwa ukisababisha uvunjifu wa amani, na ukosefu wa usalama na kusababisha hofu kwa watu, vifo na majeruhi.
2. Aidha, hata kabla ya maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ya mwaka 2018, Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika tayari zilikuwa zimefikia maazimio juu ya udhibiti wa silaha haramu katika Mkutano wa Wakuu wa nchi za Umoja wa Afrika uliofanyika kuanzia tarehe 03 – 04 Julai, 2017 Jijini Addis Ababa – Ethiopia ambapo iliazimiwa kuutangaza **mwezi Septemba kila mwaka** kuwa ni mwezi

A handwritten signature in black ink, appearing to be 'J. M. M.' followed by a flourish.

wa usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari mpaka mwaka 2030, Sambamba na kutoa msamaha kwa wahusika kutoshitakiwa endapo watasalimisha silaha hizo haramu kwa hiari na kwa muda uliopangwa.

3. Hivyo, kwa kuzingatia msingi wa Maazimio ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti Silaha na Risasi ya Mwaka 2015, Sura ya 223 na Kanuni zake za mwaka 2016 na kwa mamlaka niliyopewa chini ya Kifungu cha 64 cha Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Silaha na Risasi ya Mwaka 2015, Sura ya 223, na kwa **kuzingatia Tangazo la Serikali Namba 774 la tarehe 29/10/2021**, kwa watu wote wanaomiliki silaha kinyume na Sheria nikiwataka kusalimisha silaha hizo kwa kuzingatia masharti yafuatayo:-
  - i. Zoezi la Usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari Nchi nzima litafanyika kuanzia tarehe 1/11/2021 hadi 30/11/2021.
  - ii. Silaha hizo zisalimishwe katika Vituo vyote vya Jeshi la Polisi hapa nchini na Ofisi za Serikali za Mitaa na kwa Watendaji wa Kata kuanzia muda wa saa mbili asubuhi (2:00) hadi saa kumi jioni (10:00);
4. Nakwamba, kupitia Tangazo la Serikali Namba 774 la tarehe 29/10/2021, **Natangaza Msamaha** wa kutoshitakiwa kwa wale wote watakaosalimisha silaha kwa hiari kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa kwenye tangazo.

5. Aidha, baada ya muda uliowekwa kupita, msako mkali utafanyika kwa nchi nzima ili kuwakamata wote waliokaidi nafasi ya msamaha waliyopewa.
6. Zoezi hili litakuwa ni kwa mwezi Novemba tu, na yeyote atakayeshindwa kusalimisha silaha ndani ya muda uliotamkwa atachukuliwa kama mtuhumiwa kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu za Nchi.
7. Ntoa wito, kwa wananchi wote wanaomiliki silaha kinyume na Sheria kuhakikisha kuwa Zoezi hili linatekelezwa ipasavyo. Pia, nawasisitiza wananchi wote ambao ndugu zao walikuwa wamiliki silaha kihalali na sasa wamefariki kuhakikisha wanazisalimisha silaha hizo kulingana na masharti niliyoyataja.
8. Aidha, nawasihi Wamiliki wote wa Silaha kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya matumizi mabaya, na utunzaji mbaya wa silaha huku mkizingatia Sheria na Kanuni na yeyote atakayekiuka hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
9. Niwaombe Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambao kimsingi ni Wenyeviti wa Kamati za Usalama kuratibu zoezi hili kwa ukamilifu.
10. Pia niwaombe Viongozi wa Serikali za Mitaa na Watendaji wa Kata kutengeneza Mazingira ya kuwapokea wananchi wote watakaosalimisha silaha kwa hiari na kutoa taarifa katika Vituo vya Polisi vilivyo karibu.



11. Aidha, Nalielekeza Jeshi la Polisi kuandaa Mpangokazi wa kila siku wa kukusanya silaha zitakazosalimishwa katika Ofisi za Serikali za Mitaa na katika Ofisi za Watendaji wa Kata na kutoa taarifa ya ujumla mara zoezi hili litakapokamilika.

12. Asanteni kwa kunisikiliza.



George Boniface Simbachawene (Mb)  
**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**  
**30 OKTOBA, 2021**